MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

Na: 7. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Disemba 1-10, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Disemba 11–20, 2018

**Muhtasari**


- Mvua za *Msimu* zinaendelea vizuri kwa maeneo yanayopata msimu mmoja kwa mwaka na wakulima wanaendelea na shughuli ya upandaji mazao.
- Mvua zinazotarajiwa kwa kipindi cha tarehe 11 -20 Disemba 2018 zitasaidia katika uoteshaji na kukua kwa mazao katika maeneo mengi ya nchi.
- Wakulima wanashauriwa kuendelea kufatilia taarifa za siku kumi na kufata ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi stahiki ya mvua zinazotarajiwa
- Wafugaji wanashauriwa kutumia vizuri maji pamoja na malisho ya wanyama ili kukabiliana na upungufu unaoweza kujitokeza.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilipelekea kusukumwa kwa ukanda wa mvua wa ITCZ hadi kufika katika nchi yetu. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani lilishuhudiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi na hivyo kusababisha migandamizo midogo ya hewa. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii ilipelekea kuongeza kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kuimarisha mifumo ya mvua katika eneo la magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, baadhi ya maeneo yanayopata mvua za msimu mmoja kwa mwaka yalipata mtawanyiko hafifu wa mvua.Hata hivyo mvua za kati ya milimita 26 - 100 zilipatikana katika baadhi ya maeneo yanayozunguka kanda ya ziwa Viktoria, kanda ya kaskazini mashariki na kanda ya Pwani ya kaskazini kama inavyoonekana kwenye kielelezo. Kwa upande wa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka mvua za kiasi cha milimita kati ya 26 – 100 zilipatikana katika maeneo mengi ya magharibi,nyanda za juu kusini magharibi na upande wa kusini mwa nchi kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Disemba 1- 10, 2018

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018

Katika kipindi cha dekadi iliyopita, Mvua zilizotarajiwa ziliwezesha uchepuaji wa mazao katika maeneo mengi yanayopata mvua za msimu mmoja kwa mwaka. Katika maeneo hayo, wakulima kwa kiasi kikubwa walijishughulisha na upandaji wa mazao na kwa upande wa maeneo yanayopata mvua za misimu miwili shughuli kubwa ilikuwa ni palizi kwenye mazao.

Katika mkoa wa kagera mahindi na maharagwe yalikuwa katika hatua ya kukomaa, wakulima katika eneo hili waliendelea na shughuli za palizi kwa mazao yaliyochelewa kupandwa. Wakulima wengi katika Pwani ya kaskazini ( hususani Dar-es-salaam na Pwani) hawakuweza kupanda mazao na maeneo machache yaliyopandwa yameathirika kutokana na kukosa unyevunyevu wa kutosha ardhini.Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya Wanyama umeimarika katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za misimu miwili kwa mwaka hususani kanda ya ziwa Viktoria kutokana na mvua za Vuli zinazoendelea kunyesha.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu unayoendelea

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2018

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kupelekea kusukumwa kwa ukanda wa mvua wa ITCZ na kuwepo katika nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi na hivyo kusababisha matukio ya vimbunga hasa katika kipindi cha siku tano za mwisho. Eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuongezeka kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kuimarisha mifumo ya mvua katika eneo la magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zijazo Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) Mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo hasa katika siku tano za mwisho.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) Mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) Mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20,2018

Mvua zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua zinatarajiwa kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa uoteshaji wa mbegu zilizo katika hatua ya awali ya ukuaji. Hata hivyo mvua hizi zinatarajiwa kusaidia ukuaji wa mahindi lakini zinaweza kuleta athari kwa maharagwe yaliyokomaa katika maeneo yanayozunguka ukanda wa ziwa Viktoria hususani mkoa wa Kagera.Msimu wa mvua za Vuli unakaribia ukingoni hivyo basi wakulima wa maeneo yanayopata mvua za misimu miwili kwa mwaka wanashauriwa kutotumia mvua hizi za mwishoni mwa msimu kupanda mazao ya muda mrefu. Wakulima wanashauriwa kuendelea kufatilia taarifa za siku kumi na kupata ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi stahiki ya mvua zinazotarajiwa.Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao juu ya matumizi sahihi ya maji na malisho yaliyopo.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2018.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***